# TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA

**JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI**

# MTAALA WA SHULE ZA MSINGI

# GREDI 3

DRAFT

Chapisho la Kwanza 2017

Chapisho la Pili 2022

Chapisho la Tatu 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

ISBN:
Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

# YALIYOMO


MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ........ iv
LESSON ALLOCATION AT LOWER PRIMARY ........ vii
MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA MASOMO YA MSINGI ........ vii
KAULI KIINI ........ viii
MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI ........ viii
1.0 UZALENDO ........ 1
2.0 SHAMBANI ........ 11
3.0 MIEZI YA MWAKA ........ 20
4.0 KAZI MBALIMBALI ........ 29
5.0 USALAMA ........ 39
6.0 USAFI WA MAZINGIRA ........ 47
7.0 DUKANI ........ 53
8.0 NDEGE NIMPENDAYE ........ 60
9.0 SOKONI ........ 67
10.0 TEKNOLOJIA ........ 75
MWONGOZO WA KUTATHMINIA ........ 82
APPENDIX I: SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL) ........ 87


DRAFT

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.
   a) **Mahitaji ya kijamii**
      Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**
      Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
      Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda.
      Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa,

stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
   Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa. Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
   Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

DRAFT

**LESSON ALLOCATION AT LOWER PRIMARY**

| S/No | Learning Area | Number of Lessons |
|---|---|---|
| 1. | Indigenous Language Activities | 2 |
| 2. | Kiswahili Language Activities / Kenya Sign Language Activities | 4 |
| 3. | English Language Activities | 5 |
| 4. | Mathematical Activities | 5 |
| 5. | Religious Education Activities | 3 |
| 6. | Environmental Activities | 4 |
| 7. | Creative Activities | 7 |
| 8. | Pastoral/Religious Instruction Programme | 1 |
| **Total** | | **31** |

**MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA MASOMO YA MSINGI**

Kufikia mwisho wa masomo ya msingi, mwanafunzi aweze:

a) kutumia mbinu zifaazo za usikivu katika mawasiliano kwenye mazingira yake
b) kudhihirisha ufasaha wa dhana malimbali kusuluhisha matatizo ya kila siku,
c) kusoma kwa ufasaha na kufahamu aina zozote za maandishi ya Kiswahili
d) kuelezea mawazo, hisia na tajiriba kwa maandishi ya mkono au mbinu nyingine yoyote ya uwasilishaji
e) kutumia sarufi ipasavyo katika mawasiliano
f) kutumia msamiati ufaao katika mazingira yake kuwasiliana
g) kuonyesha ukakamavu katika kuwasilisha masuala yanayomkabili na yanayokabili mazingira yake.

**KAULI KIINI**

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya na lugha ya mawasiliano katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wakenya wengi hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ni muhimu wanafunzi wapate umilisi wa kuwasiliana kwa Kiswahili mapema hasa katika kiwango cha kwanza cha elimu. Somo hili humwezesha mwanafunzi kujenga stadi za kimsingi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Aidha, somo hili humwandaa mwanafunzi kwa mafunzo ya viwango vya juu na baadaye katika ajira.

**MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI**

Kufikia mwisho wa kiwango cha chini, mwanafunzi aweze:

a) Kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano.
b) Kuzingatia kanuni za lugha ili kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi.
c) Kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali.
d) Kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti maishani.
e) Kutumia hati za kimaandishi na mfumo wa kidijitali kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali.
f) Kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku.

**Matokeo ya Kijumla Yanayotarajiwa Katika Kiwango cha Kwanza cha Masomo**

Kufikia mwisho wa kiwango cha kwanza cha masomo, mwanafunzi aweze:

a) kutumia mbinu zifaazo za usikivu katika mawasiliano kwenye mazingira yake
b) kudhihirisha ufasaha wa kuzungumza kwa Kiswahili
c) kusoma kwa ufasaha na kufahamu aina zozote za maandishi ya Kiswahili
d) kuelezea mawazo, hisia na tajiriba kwa maandishi ya mkono au mbinu nyingine yoyote ya uwasilishaji
e) kutumia sarufi ipasavyo katika mawasiliano
f) kutumia msamiati ufaao katika mazingira yake kuwasiliana
g) kuonyesha ukakamavu katika kuwasilisha masuala yanayomkabili na yanayokabili mazingira yake.

**MADA**

1. Kusikiliza na Kuzungumza
2. Kusoma
3. Kuandika
4. Sarufi

**MASUALA**

5. Uzalendo
6. Shambani
7. Miezi ya Mwaka
8. Kazi Mbalimbali
9. Usalama
10. Usafi wa Mazingira
11. Dukani
12. Ndege Nimpendaye
13. Sokoni
14. teknolojia

## 1.0 UZALENDO

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Maamkuzi na Maagano**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maamkuzi na maagano mbalimbali yatumiwayo katika jamii,<br>b) kutumia ipasavyo maamkuzi na maagano mbalimbali yatumiwayo katika jamii,<br>c) kuthamini matumizi ya maamkuzi na maagano katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yanayotumiwa katika maamkuzi na maagano *(k.v. Umeamkaje? Umeshindaje? Safiri salama, mchana mwema, usiku mwema)* kutoka kwenye chati, vitabu, kadi maneno, mti maneno, michoro, picha au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kujadili na wenzake picha, michoro, video n.k. zinazoonyesha vitendo vya maamkuzi na maagano,<br>● kuigiza maamkuzi na maagano akiwa na wenzake ili kujenga umilisi wa kutumia maneno haya,<br>● kujadiliana na mzazi au mlezi wake maamkuzi na maagano kutoka kwa jamii yake. | Je, unajua maamkuzi na maagano yapi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki na kuwasiliana na wenzake katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji.
- Uraia – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli mbalimbali za kikundi.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposikiliza kwa makini maamkuzi na maagano mbalimbali kutoka kwenye vifaa vya kidijitali.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika mijadala ya maamkuzi na maagano darasani.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Upendo – mwanafunzi anapozingatia maamkuzi na maagano katika jamii.
- Heshima – anapotumia maneno ya heshima na adabu katika maamkuzi na maagano.

**Masuala Mtambuko**

Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anapojadiliana na mzazi au mlezi wake maamkuzi na maagano kutoka kwa kijamii yake.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia maamkuzi na maagano.

DRAFT

| 1.0 UZALENDO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa ufahamu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno 51- 54 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v. uzalendo, umoja, undugu, ushirikiano, upendo)* akiwa na wenzake,<br>• kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>• kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>• kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>• kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>• kueleza mafunzo yanayotokana na | 1. Je, unapenda kusoma hadithi za aina gani?<br>2. Je, ni mambo gani unayoweza kujifunza kutokana na hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuimarisha stadi ya kusoma. | kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi kutambua msamiati kuhusu suala lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali katika shughuli za ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposoma kifungu ili kuimarisha stadi ya kusoma.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapojadili picha ,kutabiri na kudhibitisha utabiri kuhusu hadithi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotoa hoja zake kwa wenzake na anaposhirikisha mzazi au mlezi wake kusoma na kujadili kifungu.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.
- Heshima – mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kusoma kifungu darasani.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotoa muhtasari wa hadithi aliyoisoma.

**Masuala Mtambuko**

- Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.
- Usalama wa mtandaoni – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma ufahamu kuhusu suala lengwa na kuzingatia usalama mtandaoni.
- Haki na majukumu ya kibinadamu – mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza katika

DRAFT

| |
|---|
| shughuli za kikundi wakiwepo walio na changamoto za kimaumbile. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufahamu. |

| 1.0 UZALENDO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo yanayozingatiwa kufanikisha hati nadhifu,<br>b) kuandika kifungu cha maneno kati ya 25-30 kwa hati nadhifu,<br>c) kufurahia kuandika kwa hati nadhifu ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mambo mbalimbali yanayozingatiwa kufanikisha hati nadhifu *(k.v. muundo wa herufi, nafasi ifaayo kati ya maneno, nafasi zifaazo pambizoni, kutenganisha sentensi ifaavyo, usafi wa nakala )* kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu cha maneno yasiyozidi 30 kwa hati nadhifu kutoka kwenye kitabu, chati au vifaa vya kidijitali,<br>● kuandika kifungu cha maneno yasiyozidi 30 akizingatia hatua za uandishi *(k.v. maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi)* na kuwasomea wenzake. | Unazingatia mambo gani unapoandika kifungu? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mambo ya kuzingatiwa ili | | | | |

DRAFT

kufanikisha hati nadhifu.

- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli mbalimbali za kuandika.
- Ubunifu – mwanafunzi anaponakili kifungu cha maneno kwa hati nadhifu.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.
- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kwa utulivu.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali.

**Masuala Mtambuko**

Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa.

| 1.0 UZALENDO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Matumizi ya yeye na wao**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua neno **yeye** na **wao** katika sentensi,<br>b) kutumia neno **yeye** na **wao** ipasavyo katika sentensi,<br>c) kufurahia kutumia neno **yeye** na **wao** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaohusu **yeye** na **wao** kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua neno **yeye** na **wao** kutoka kifungu alichokisikiliza,<br>● kusoma vifungu na kutambua neno **yeye** na **wao** akiwa na wenzake au katika kikundi,<br>● kujaza mapengo kwa kutumia **yeye** na **wao,**<br>● kutumia **yeye** na **wao** katika kuigiza mazungumzo na wenzake katika kikundi k.v. *Yeye anasoma - wao wanasoma.* | Ni maneno gani unayoyatumia kuwataja wenzako bila kutumia majina yao halisi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kutoa mifano kwa kutumia **yeye** na **wao**.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **yeye** na **wao**.

DRAFT

| |
|---|
| ● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya **yeye** na **wao**.<br>● Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kutumia yeye na **wao** ifaavyo. |
| **Maadili**<br>● Heshima – mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi.<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi huku akisikiliza michango yao na kutoa maoni. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maneno lengwa.<br>● Uraia – mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● Engilish Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia nafsi.<br>● Enviromental Activities – somo hili linashughulikia kujitambua na kutambua wengine.<br>. |

| 2.0 SHAMBANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Matamshi Bora**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vokali za Kiswahili katika matini,<br>b) kutamka ipasavyo vokali za Kiswahili katika matini, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vokali za Kiswahili katika matini ya kutamkwa au kuandikwa,<br>● kutamka ipasavyo vokali za Kiswahili,<br>● kutambua konsonanti za Kiswahili katika matini ya kutamkwa au kuandikwa,<br>● kutamka ipasavyo konsonanti za Kiswahili,<br>● kusikiliza vokali na konsonanti za Kiswahili (a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i, j, k, l, m, n,ng, ng', ny, o, p, | Je, kwa nini ni muhimu kutambua sauti za lugha fulani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | c) kutambua konsonanti za Kiswahili katika matini,<br>d) kutamka ipasavyo konsonanti za Kiswahili katika matini,<br>**e)** kuchangamkia kutamka sauti za Kiswahili ili kuboresha matamshi. | r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z) zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kutambua vokali na konsonanti,<br>● kutambua vokali na konsonanti za Kiswahili katika kifungu kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutamka maneno, sentensi au kifungu chenye sauti za Kiswahili akiwa na wenzake,<br>● kujirekodi akitamka sauti za Kiswahili akitumia vifaa vya kidijitali na kujitathmini pamoja au kutathminiwa na wenzake,<br>● kutamka sauti za kiswahili ipasavyo naye mzazi au mlezi ampe maoni yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuzisikiliza, kuzitambua na kuzitamka vokali na konsonanti za Kiswahili.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza vokali na konsonanti za Kiswahili na kujirekodi akizitamka.
- Kujiamini – mwanafunzi anapozitamka vokali na konsonanti za Kiswahili kwa mzazi au mlezi wake ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapokuwa makini kusikiliza vokali na konsonanti zikitamkwa na mwalimu.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wanzake katika shughuli za kutamka vokali na konsonanti za Kiswahili kwenye kikundi kwa utulivu.<br>● Heshima – mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake wakiwemo walio na changamoto za kimaumbile.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali alivyotumia katika kujirekodi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Elimu ya mazingira na tabianchi – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka vokali na konsonanti za Kiswahili kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia suala la matamshi bora. |

| 2.0 SHAMBANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti lengwa (/bw/, /fy/, /kw/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 47 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi) akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake,<br>• kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, n.k. akiwa na | Je, utafanya mambo gani unaposoma ili uweze kusikika vizuri? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zifaazo,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma kwa ufasaha akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali katika shughuli za ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa huku akizingatia matamshi bora, sauti inayosika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua sauti lengwa kwa ufasaha na kutumia vifaa vya kidijitali.
- Heshima – mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za darasani.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali anachotumia kujifunzia.

**Masuala Mtambuko**

- Usalama mtandaoni – mwanafunzi anaposoma hadithi yenye sauti lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama.
- Elimu ya mazingira na tabianchi – mwanafunzi anaposoma kifungu na wenzake kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo pia yanashughulikia dhana ya kusoma kwa ufasaha.

| 2.0 SHAMBANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi kubwa katika matini,<br>b) kuandika kifungu cha hadithi akitumia herufi kubwa ifaavyo,<br>c) kufurahia kuandika kwa kuzingatia herufi kubwa katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua herufi kubwa katika kifungu kilichoko kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa,<br>● kuandika kifungu chenye maneno **25-30** akizingatia maumbo ya herufi kubwa ifaavyo akizingatia hatua za uandishi (*maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi)*na kuwasomea wenzake,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichokiandika akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa ili | Kwa nini tunatumia hati nadhifu kati uandishi ? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kuandika kifungu kwa kutumia herufi kubwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia maumbo ya herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi wake kifungu alichokiandika akitumia maumbo ya herufi kubwa.
- Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kuandika maumbo ya herufi kubwa ipasavyo.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika kifungu.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Amani – mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake kutathmini herufi kubwa alizoziandika.

**Masuala Mtambuko**

Masuala ya kijamii na kiuchumi – mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia herufi kubwa ipasavyo.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kuandika herufi kubwa.

DRAFT

| 2.0 SHAMBANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Umoja na Wingi wa Sentensi**<br><br>*(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sentensi katika umoja na wingi,<br>b) kutunga sentensi katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia umoja na wingi katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake*(k.v. mimi ninapanda mti- sisi tunapanda miti, mimi ninapenda kulima - sisi tunapenda kulima),*<br>● kusoma sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>● aambatanishe umoja na wingi wa sentensi alizopewa kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali, n.k. akiwa na wenzake,<br>● kuigiza michezo inayohusisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi katika umoja na wingi wa sentensi akiwa na wenzake, | Je, kwa nini unahitaji kutaja vitu katika hali ya umoja na wingi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kuwasiliana na mzazi au mlezi akitumia sentensi katika hali ya umoja na wingi ipasavyo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , na kuchangia kikamilifu katika kuandika sentensi katika umoja na wingi.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoeleza kuhusu vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotunga sentensi katika umoja na wingi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapowasiliana na mzazi au mlezi akitumia sentensi katika hali ya umoja na wingi katika mazungumzo ya kila siku.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma sentensi katika hali ya umoja na wingi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza nyenzo zinazotumiwa katika ujifunzaji wa sentensi za umoja na wingi.
- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi akizingatia suala lengwa.
- Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wengine wanapotambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye matini.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia nomino.

| 3.0 MIEZI YA MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Maneno ya Heshima na Adabu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima na adabu katika matini,<br>b) kutumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano,<br>c) kuthamini matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama michoro, picha au video inayowasilisha vitendo vya heshima na adabu akiwa na wenzake,<br>● kutambua maneno ya adabu na heshima kutoka kwa michoro, picha au video aliyotazama (tasfida) *k.v. kwenda msalani, haja kubwa, haja ndogo, kuendesha*<br>● kuigiza mazungumzo yanayoonyesha matumizi ya maneno ya heshima na adabu akishirikiana na wenzake,<br>● kujadiliana na mzazi au mlezi maneno ya heshima na adabu katika jamii yake. | Je, ni kwa nini tunatumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama picha, michoro na video kuhusu maneno heshima na adabu.<br>● Ubunifu – mwanafunzi anapoigiza kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotambua baadhi ya maneno ya adabu na heshima na matumizi yake. |
| **Maadili**<br>● Heshima – mwanafunzi anapotumia maneno ya adabu na heshima ipasavyo.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali ipasavyo.<br>● Amani – mwanafunzi anapotumia maneno ya adabu na heshima katika mawasiliano.<br>● Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutazama video bila kuzozana.<br>● Uadilifu – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika maigizo ya mazungumzo ya maneno ya adabu na heshima. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Mahusiano ya kijamii – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kuigiza maneno ya heshima na adabu. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities, Indigenous Language Activities na Religious Education Activities – masomo haya yanashughulikia dhana ya heshima na adabu. |

| 3.0 MIEZI YA MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea tokea katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza au kutazama nyimbo kuhusu majina ya miezi ya mwaka kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutaja majina ya miezi ya mwaka akiwa na wenzake,<br>● kuimba nyimbo kuhusu majina ya miezi akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 55 - 60 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v. Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Novemba, Disemba)* akiwa na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>● kushirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka, | Je, ni mambo yapi unaweza kujifunza kutokana na unachokisoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | stadi ya kusoma. | ● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kufafanua mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>● kumsomea mzazi au mlezi majina ya miezi ya mwaka aliyojifunza ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi na kushiriki kikamilifu katika kutabiri kitakachotokea katika hadithi.
- Uraia – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi kueleza ujumbe wa kifungu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali katika shughuli za ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi kusoma na kujadili kifungu kuhusu suala lengwa.
- Ubunifu – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe katika kifungu.
- Upendo – mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya kifaa vya kidijitali darasani.

| |
|---|
| ● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anachotumia kujifunzia.Pia anapotekeleza majukumu aliyopewa anapofanya maigizo kuhusu miezi ya mwaka.<br>● Haki za kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuimba nyimbo kuhusu suala lengwa.<br>● Amani – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu katika shughuli za kusoma kifungu. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mahusiano ya kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka ukakamavu wake unajengeka. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia stadi ya kusoma. |

DRAFT

| 3.0 MIEZI YA MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi ndogo zilizoandikwa ipasavyo katika kifungu,<br>b) kuandika kifungu akitumia herufi ndogo ifaavyo,<br>c) kufurahia kuandika kwa kuzingatia herufi ndogo ifaavyo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi ndogo kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua herufi ndogo zilizoandikwa ifaavyo katika kifungu kilichoko kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,<br>● kuandika kifungu chenye maneno 55-60 akizingatia maumbo ya herufi ndogo ifaavyo akizingatia hatua za uandishi *(maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji,*<br>*nakala safi)* na kuwasomea wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,<br>● kuwaonyesha wenzake kifungu alichoandika akizingatia maumbo ya | Je, unazingatia mambo gani unapoandika herufi ndogo ifaavyo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | herufi ndogo ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu jinsi ya kuendeleza herufi ndogo.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kutumia kifaa cha kidijitali kutazama kielelezo cha uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi ndogo.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika kifungu kifupi akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,
- Kujiamini – mwanafunzi anapowaonyesha wenzake kazi aliyoandika ili waitolee maoni.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu mada lengwa kwa kutumia herufi ndogo.

**Masuala Mtambuko**

Mahusiano ya kijamii – mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Languages Activities – masomo haya pia yanashughulikia stadi ya kuandika.

Mathematics Activities – somo hili pia linashughulikia mada ya miezi ya mwaka.

| 3.0 MIEZI YA MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Matumizi ya neno yule na wale** *(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya neno **yule** na **wale** katika kifungu,<br>b) kutumia neno **yule** na **wale** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya neno **yule** na **wale** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya neno **yule** na **wale** kutoka kwenye chati, kitabu, vyombo vya kidijitali nk. akiwa na wenzake,<br>● kusilikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya neno **yule** na **wale** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kujadili matumizi yake akiwa na wenzake,<br>● kusoma sentensi zilizotumia neno **yule** na **wale** kutoka kwenye chati, kitabu, vifaa vya kidijitali akiwa akiwa na wenzake,<br>● kuigiza vitendo vya kuwaashiria watu mbalimbali kwa kutumia neno **yule** na **wale** akiwa na wenzake,<br>● kuandika sentensi akitumia **yule** na **wale (***k.v Mtoto* | Unaweza kutunga sentensi zipi ukitumia maneno **yule** na **wale**? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *yule anacheza - watoto wale wanacheza)* na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili akamilishe sentensi akitumia **yule** na **wale,**<br>● kumsomea mzazi au mlezi kazi aliyoandika kuhusu matumizi ya **yule** na **wale.** | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia maneno **yule** na **wale**.
- Kujiamini – mwanafunzi anapoigiza matumizi ya neno **yule** na **wale** akishirikiana na wenzake katika kikundi.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia neno **yule** na **wale** kwa lugha fasaha.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kwa kutumia neno **yule** na **wale**.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia neno **yeye** na **wao.**
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kikundi.

**Masuala Mtambuko**

Masuala ya kijamii na kiuchumi – mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

| 4.0 KAZI MBALIMBALI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Matamshi Bora**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (*/py/, /vy/, /sh/*) katika matini mbalimbali (*k.v kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali)*<br>● kutumia kifaa cha kidijitali *(k.v. kupitia programu ya papaya)* kusikiliza matamshi bora ya sauti lengwa,<br>● kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali k.*v. kinasasauti na rununu* akiwa na wenzake kisha | Unazingatia mambo gani unapotamka maneno mbalimbali katika kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | azitamke,<br>● kusikiliza maneno yenye sauti lengwa yakisomwa na mwalimu kisha atambue sauti lengwa katika maneno hayo,<br>● kutamka maneno yenye sauti ifaavyo akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kutoka kwa kitabu au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Uraia – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wa jamii mbalimbali katika kutekeleza shughuli za kikundi.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana katika kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima – mwanafunzi anapoheshima matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Amani – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu katika kutambua silabi za sauti lengwa.



DRAFT

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>• Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali kusoma kifungu chenye maneno ya sauti /*py*/,/*vy*/ na /*sh*/ kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya kifedha – mwanafunzi anaposoma na kutunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia suala la matamshi bora. |

DRAFT

| 4.0 KAZI MBALIMBALI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **4.2 Kusoma** | **4. 2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo<br>e) kusoma kifungu | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa (*/py/, /vy/, /sh/)* katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 49 kwa dakika na kwa | Je, unahakikishaje umesoma kifungu kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | kuizingatia viakifishi) akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake ,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika,kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika kutambua sauti lengwa na kusoma kifungu.
- Uraia – mwanafunzi anapotangamana na wenzake kusoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotambua sauti lengwa katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa.
- Kujithamini – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akitumia matamshi bora,sauti inayosikika,kasi ifaayo na ishara zifaazo.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua sauti na kusoma kifungu.
- Heshima – mwanafunzi anapothamini wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu cha maneno yenye sauti lengwa.
- Upendo – mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji.

DRAFT

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>Elimu ya kifedha – mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Indigenous Language Activities na English Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufahamu. |

DRAFT

| 4.0 KAZI MBALIMBALI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Nafasi ya Pambizo katika uandishi** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nafasi ya pambizo na nafasi ya kuzingatia anapoandika aya,<br>b) kuandika kifungu cha maneno yasiyozidi 60 akizingatia pambizo na aya,<br>c) kufurahia kuandika kifungu akizingatia pambizo na aya. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua nafasi ya pambizo na nafasi ya kuzingatia anapoandika aya akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu na kutambua pambizo na aya kwenye kitabu, chati, kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kuandika kifungu akizingatia pambizo na aya kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali na kuwasomea wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo na kuwasomea wenzake,<br>● kuandika na kumuonyesha | Je, kwa nini tuzingatie nafasi za pambizo tunapoandika? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mzazi au mlezi kifungu alichoandika akizingatia aya na pambizo ili ampe maoni yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa chakidijitali kuandika kifungu akizingatia aya na pambizo.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichoandika akizingatia aya na pambizo ipasavyo.
- Kujiamini – mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia aya na pambizo na kuwasomea wenzake.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji na kuheshimu maoni yao.
- Uzalendo – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo.

**Masuala Mtambuko**

- Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akizingatia pambizo na aya.
- Elimu ya kifedha – mwanafunzi anaposoma kifungu kifupi na wenzake kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kuandika kwa kuzingatia pambizo na aya.

| 4.0 KAZI MBALIMBALI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Umoja na Wingi wa Sentensi**<br><br>*(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sentensi katika umoja na wingi,<br>b) kuandika sentensi katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia umoja na wingi katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma sentensi katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake ,<br>● kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye chati au vifaa vya kidijitali,<br>● kujaza nafasi kwa kukamilisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na mwenzake,<br>● kushiriki katika mchezo wa kusoma sentensi katika umoja na mwenzake,<br>● kuandika umoja na wingi wa sentensi akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizoandika katika umoja na wingi ili azitolee maoni. | Je, utajua vipi kama sentensi imeandikwa katika umoja au wingi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika sentensi katika umoja na wingi.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapokamilisha sentensi katika umoja na wingi.

| |
|---|
| ● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi.<br>● Kujiamini – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi sentensi alizoandika katika umoja na wingi. |
| **Maadili**<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi katika umoja na wingi.<br>● Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapoandika umoja na wingi wa sentensi.<br>● Haki za jamii – mwanafunzi aanaposhiriki katika mchezo wa kutunga sentensi kwa umoja na wingi na wenzake. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya kifedha – mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi zinazohusiana na mapato ya watu na kazi mbalimbali. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Languages Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia dhana ya umoja na wingi. |

DRAFT

| 5.0 USALAMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe unaowasilishwa katika kifungu,<br>b) kutambua msamiati uliotumiwa katika kifungu alichosikiliza,<br>c) kutunga sentensi kutumia msamiati uliotumika kwenye kifungu alichosikiliza,<br>d) kusimulia upya kifungu cha hadithi alichokisikiliza,<br>e) kuchangamkia kusikiliza kifungu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza kifungu cha maneno 60-65 kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali ili kutambua ujumbe unaowasilishwa,<br>● kutambua msamiati uliotumika katika ufahamu aliousikiliza akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi kwa kutumia msamiati aliousikiliza uliotumika kwenye kifungu,<br>● kujibu maswali yanayohusiana na kifungu alichosikiliza,<br>● kujadili mambo muhimu katika kifungu alichokisikiliza akiwa na wenzake,<br>● kusimulia wenzake upya kifungu alichokisikiliza, | Je, unazingatia mambo gani ili kuelewa mambo unayoelezewa? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na kuwasiliana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za huduma kwa jamii kwa kusimulia visa vyepesi.
- Kujiamini – mwanafunzi anaposimulia upya kifungu alichokisikiliza.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Upendo – mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anaposimulia wenzake upya kifungu alichokisoma. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Masuala ya usalama – mwanafunzi anaposikiliza na kuzungumzia masuala ya usalama. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusikiliza na kuzungumza.<br>● Enviromental Activities – somo hili pia linashughulikia suala la usalama. |

| **5.0 USALAMA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza au kutazama nyimbo kuhusu usalama shuleni kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutaja masuala ya usalama shuleni akiwa na wenzake,<br>● kuimba nyimbo kuhusu usalama shuleni akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 60- 65 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v. usalama, hatari, umia, tibu, tahadhari, zahanati, dawa, huduma ya kwanza)* akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha | Je, ni mambo gani unapaswa kuzingatia ili kufanikisha usomaji bora? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | ufahamu akiwa na wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu usalama shuleni,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akiwa na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa kutunga sentensi kwa usahihi kwa kuzingatia suala lengwa na masuala mtambuko mbalimbali,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu usalama wake shuleni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia kikamilifu katika kazi za kikundi wanapojadili ujumbe wa kifungu na kutabiri kitakachotokea katika hadithi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposoma matini mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusoma.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia msamiati wa suala lengwa.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapofanya utabiri kutokana na picha.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadiliana kuhusu ujumbe katika kifungu.
- Heshima – mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu na kutabiri.
- Uadilifu – mwanafunzi anapowashirikisha wengine kufanya maigizo kuhusu usalama shuleni.

**Masuala Mtambuko**

- Mshikamano wa jamii – mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi na kutoa mchango wake, ukakamavu wake unajengeka.
- Masuala ya usalama – mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu masuala ya usalama.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufahamu.

DRAFT

- Enviromental Activities – somo hili pia linashughulikia masuala ya usalama.

DRAFT

| 5.0 USALAMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Matumizi ya Kiulizi**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alama ya kiulizi katika maandishi,<br>b) kueleza matumizi ya alama ya kiulizi katika maandishi,<br>c) kuandika kifungu cha maneno kati ya 55-60 akitumia alama ya kiulizi ipasavyo,<br>d) kufurahia kutumia kiulizi katika maandishi ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua alama ya kiulizi kutoka kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kujadili na wenzake matumizi ya alama ya kiulizi ili kukuza uwezo wa kuitumia ipasavyo,<br>● kunakili ipasavyo kifungu kilichotumia alama ya kiulizi akishirikiana na wenzake,<br>● kuandika kifungu cha maneno kati ya 55-60 akizingatia matumizi ya alama ya kiulizi kisha kuwasomea wenzake ili waitolee maoni. | Je, alama ya kiulizi inatumika vipi katika uandishi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapowasomea kifungu alichoandika kwa kutumia alama kiulizi.
- Ubunifu – mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu kwa kutumia alama ya kiulizi ipasavyo.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji na kuheshimu maoni yao.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotumia alama ya kiulizi katika maandishi na pia anapotumia vifaa vya kidijitali.

**Masuala Mtambuko**

- Usalama mtandaoni – mwanafunzi anapoelekezwa kutangamana na mitandao ya kijamii kwa njia salama.
- Masuala ya usalama – mwanafunzi anapoandika kifungu chepesi kuhusu suala la usalama.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia matumizi ya kiulizi.
- Mathematics Activities – soma hili pia linashughulikia matumizi ya kiulizi.

DRAFT

| 5.0 USALAMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.4 Sarufi** | **5.4.4. Matumizi ya -ake na -ao** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **-ake** na **-ao** katika mawasiliano,<br>b) kutumia **-ake** na **-ao** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia **-ake** na **-ao** ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya -**ake** na **–ao** kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno au chati akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaotumia –**ake** na –**ao** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa, au vifaa vya kidijitali,<br>● kusoma kifungu kilichotumia **-ake** na **-ao** akiwa na wenzake,<br>● kuigiza matumizi ya **-ake** na **-ao** akiwa na wenzake katika kikundi kwa kutumia vitu anavyomiliki k.v; *kiti chake – viti vyao,*<br>● kutunga sentensi akitumia -**ak**e na -**ao** na kuzijadili na mwenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zilizotumia **-ake** na-**ao,**<br>● kumtungia mzazi au mlezi sentensi zilizo na **-ake** na -**ao** kwa kurejelea vitu mbalimbali nyumbani. | Je, -**ake** na -**ao** hutumiwa vipi katika mawasiliano? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi akitumia **-ake** na **-ao**.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kutumia **-ake** na **–ao** kwa kurejelea vitu mbalimbali nyumbani.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya**-ake** na **-ao**.
- Ubunifu – mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi kwa kutumia **-ake** na **-ao**.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Heshima – mwanafunzi anapoheshimu michango ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapochukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Masuala ya usalama – mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia **-ake** na **-ao**. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia sarufi. |

DRAFT

| 6.0 USAFI WA MAZINGIRA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifungu kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye sauti lengwa katika matini,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (*/dh/, /th/* na */ch/*) katika kitabu, kadi maneno, chati, mti maneno, vifaa vya kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kuyatamka ipasavyo,<br>● kuambatanisha silabi na kutamka maneno yanayotokana na sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kutambua | 1. Je, matamshi bora hufanikisha vipi mawasiliano?<br>2. Je, ni mambo gani yanayozingati-wa ili kuboresha matamshi? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kwa sauti kifungu kifupi kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa,<br>● kujirekodi akisoma kifungu kilicho na maneno yaliyo na sauti lengwa na kusikiliza na wenzake ili kuitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapoambatanisha silabi na kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.

**Maadili**

- Haki za jamii – mwanafunzi aposhirikiana na wenzake katika kutamka maneno ya silabi za sauti lengwa.
- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Amani – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kupotambua silabi za sauti lengwa.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anaposoma kifungu kifupi kinachohusu usafi wa mazingira akizingatia silabi za sauti lengwa na matamshi bora.
- Usalama mtandaoni – mwanafunzi anapotambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia suala la matamshi bora.

DRAFT

| 6.0 USAFI WA MAZINGIRA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa (/dh/, /th/ na /ch/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake ,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 51 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi),<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akishirikiana na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | Je, utafanya nini ili kusikika vizuri unaposoma? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia katika kutambua sauti na kusoma kifungu.
- Uraia – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi bila ubaguzi.
- Kujiamini – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu cha maneno kuhusu suala lengwa.

| |
|---|
| ● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali kusoma hadithi kwa kutumia matamshi bora. |
| **Maadili**<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa.<br>● Upendo – mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali kusoma hadithi.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anaposoma hadithi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Indigenous Language Activities na English Language Activities – masomo haya pia hushughulikia kusoma kwa ufasaha. |

| **6.0 USAFI WA MAZINGIRA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Imla**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yanayotamkwa kwenye imla ili kuyaandika ipasavyo,<br>b) kuandika kifungu cha maneno 55-60 yanayotamkwa kwenye imla akizingatia kanuni za uandishi zifaazo,<br>c) kuchangamkia kuandika kifungu akitumia maneno yanayotamkwa kwa kuzingatia kanuni zifaazo za uandishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yanayotamkwa yakizingatia suala na sauti /**dh**/, /**th**/ na /**ch**/ na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali kutoka kwenye kitabu, chati, kapu la maneno n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini maneno yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali ili kuyaandika ipasavyo,<br>● kuandika kifungu cha maneno 55-60 yatakayotamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika vifaa vya kidijitali n.k. akizingatia kanuni za zifaazo za uandishi (*k.v matumizi ya herufi kubwa na ndogo, tahajia, nafasi* | Unaposomewa chochote ili ukiandike,utafanya nini ili uandike ifaavyo ? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *baina ya maneno n.k*),<br>● kujadili na wenzake kifungu alichokiandika ili kukitathmini,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu alichokiandika akizingatia kanuni za uandishi zifaazo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapowaeleza wenzake maneno katika kifungu cha imla.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu cha imla akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kuandika maneno na kifungu cha imla.
- Kujiamini – mwanafunzi anapofaulu kuandika imla kwa kutumia maneno yenye sauti lengwa.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.
- Upendo – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapoandika kifungu cha maneno 55-60 yatakayotamkwa.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anapoandika kifungu cha maneno yatakayotamkwa kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kanuni zifaazo za maandishi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Languages Activities – masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa imla.

**6.0 USAFI WA MAZINGIRA**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Matumizi ya -eupe, - eusi,** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** kwa kurejelea vitu | Je, vitu katika mazingira yako yana rangi gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **- ekundu**<br><br>(*Vipindi 3*) | yenye **- eupe, -eusi** na **- ekundu** ili kuyatumia ipasavyo katika mawasiliano,<br>b) kutumia**-eupe, - eusi, -ekundu** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia **-eupe, -eusi, -ekundu** katika mawasiliano ya kila siku. | halisi katika mazingira yake, kitabu, chati, vifaa vya kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maelezo kuhusu matumizi ya, **-eupe, -eusi, -ekundu** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake ,<br>● kusoma sentensi zinazotumia maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zenye matumizi ya -**eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapotumia **-eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake kutunga sentensi .
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza matumizi ya **-eupe, -eusi, - ekundu**.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga akitumia **-eupe, -eusi, -ekundu**.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotumia maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** kutunga sentensi.

**Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anapotangamana na wenzake kwa heshima katika shughuli za kikundi.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotekeleza shughuli za darasani.

**Masuala Mtambuko**

Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa.

DRAFT

| Uhusiano na Masomo Mengine |
|---|
| English Language Activities and Indigeneous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia vivumishi. |

| 7.0 DUKANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Maagizo**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maagizo mepesi yanapotolewa darasani,<br>b) kutoa na kufuata maagizo mepesi yanayotumiwa darasani,<br>c) kufurahia kuzingatia maagizo katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua aina mbalimbali za maagizo kwenye kitabu, chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake katika kutoa na kufuata maagizo mepesi kama vile *k.v. simama uende uufungue mlango,*<br>● kutazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua aina mbalimbali za maagizo akiwa na wenzake,<br>● kushiriki katika mjadala wa maagizo yafaayo na yasiyofaa kufuatwa akiwa na wenzake,<br>● kuimba nyimbo na kukariri mashairi mepesi yanayohusu maagizo akiwa na wenzake,<br>● kuigiza maagizo mepesi akiwa na wenzake,<br>● kumwimbia mzazi au mlezi wake wimbo unaoashiria maagizo ili atoe maoni yake. | Je,ni kwa nini mtu hufuata yale anayoambiwa? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa** |
| --- |
| ● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika masimulizi na wenzake ya kufuata na kutofuata maagizo.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotoa maoni katika majadiliano kuhusu jinsi ya kufuata maagizo.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.<br>● Ubunifu – mwanafunzi anapoigiza maagizo mepesi akishirikiana na wenzake. |
| **Maadili**<br>● Amani – mwanafunzi anapofanya kazi katika kikundi na wenzake kwa utulivu.<br>● Umoja – mwanafunzi anapofanya kazi na wenzake kwa upole na kuelewana.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali.<br>● Uadilifu – mwanafunzi anapotazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo kutoka kwenye kifaa cha kidijitali bila usimamizi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Elimu ya kifedha – mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu matumizi ya pesa dukani. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia stadi za kusikiliza na kuzungumza. |

| **7.0 DUKANI** | | | | |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **7.2. Kusoma** | **7.2.1 Kusoma kwa Ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutaja majina ya vitu vinavyopatikana dukani akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 65 - 70 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v duka, bidhaa, pesa, uza, nunua, chenji, mteja, muuzaji)* akiwa na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kufanya maigizo baina ya muuzaji na mnunuzi,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama | Je, unazingatia mambo gani unaposoma kifungu cha hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | picha kwenye kitabu akiwa na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi akizingatia picha akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu kifungu baada ya kukisoma,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kazi ya kikundi na kushiriki kikamilifu wanapotabiri na kujadili ujumbe katika kifungu.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotoa na kuthibitisha utabiri wake kuhusu kitakachotokea katika hadithi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili picha na kutabiri kitakachotokea katika hadithi.
- Haki za kijamii – mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotabiri kilichotokea katika kifungu alichokisoma.
- Amani – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo baina ya mnunuzi na mwuzaji.

**Masuala Mtambuko**

Elimu ya kifedha – mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu masuala yanayohusiana na shughuli za dukani.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

Indigenous Language Activities na English Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufahamu.

## 7.0 DUKANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Uandishi wa Insha** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>b) kuandika kisa cha kati ya maneno 85-90 kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa kisa *(k.v.wahusika,ujumbe,muundo),*<br>● kusikiliza kisa kikitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>● kusoma kielelezo cha insha kwenye kitabu, chati au katika kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutambua kanuni muhimu za uandishi (*k.v. hati nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.*),<br>● kuandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa na kujadili na wenzake; kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake,<br>● kumsomea kifungu kisha amwonyeshe mzazi au mlezi. | Je, ni mambo gani tunazingatia katika uandishi wa insha? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki na kujadili na wenzake kutambua vipengele vya uandishi wa insha.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika insha.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika kifungu.
- Ubunifu – mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa na kujadili na wenzake.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.

DRAFT

| |
|---|
| ● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mahusiano ya kijamii – mwanafunzi anapowathamini wenzake na kushirikiana katika shughuli za uhariri.<br>● Masuala ya kifedha – mwanafunzi anapoandika ufahamu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – Masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa insha. |

DRAFT

| 7.0 DUKANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Ukanushaji wa nafsi ya tatu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi,<br>b) kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi kwa usahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno, chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kutambua ukanushaji wa nafsi hiyo,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi<br>● kutunga sentensi akitumia nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji wake (*kwa mfano: yeye anaandika - yeye haandiki),*<br>● kuigiza matumizi ya nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi sentensi za nafsi ya tatu umoja na wingi zilizokanushwa kuashiria vitendo vya watu mbalimbali nyumbani. | Unafikiri mwalimu wako alifanya nini jana? Kama hakufanya mambo uliyotaja ungesemaje? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki kutunga sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji wake.
- Kujiamini – mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi katika kikundi akitumia ukanushaji wa nafsi lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza wimbo au kifungu kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja

| |
|---|
| **Maadili**<br>Heshima – mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza wimbo au kifungu kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu.<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu katika shughuli za kikundi.<br>● Haki za jamii – mwanafunzi anapokanusha sentensi za nafsi ya tatu kuashiria vitendo vya watu mbalimbali nyumbani. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za ukanushaji.<br>● Masuala ya kifedha– mwanafunzi anapotumia ukanushaji katika sentensi zinazolenga masuala ya dukani. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Engilish Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia nafsi. |

DRAFT

| 8.0 NDEGE NIMPENDAYE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Matamshi Bora**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (/**mbw**/,/**nd**/, /**ny**/) katika kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kutambua silabi lengwa,<br>● kutamka maneno aliyosikiliza yenye sauti lengwa; atamke na mwalimu na mwishowe atamke akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu cha hadithi na kutambua sauti lengwa,<br>● kusoma kwa sauti kifungu kilicho na sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>● kujirekodi akisoma hadithi zilizo | Je, matamshi bora hukuzwa kwa njia gani? |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | na maneno yenye sauti lengwa na kujisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi, | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli mbalimbali ili kuboresha matamshi yake.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno yenye sauti lengwa na azisikilize na wenzake ili kutathmini matamshi.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana , kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima – mwanafunzi anapothamini matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo – mwanafunzi anapowashirikisha wenzake katika matumizi ya vifaa vya kidijitali.

**Masuala Mtambuko**

Elimu ya utunzaji wa wanyama – mwanafunzi anaposoma kifungu kilicho na sauti ***mbw, nd*** na ***ny*** kuhusu suala lengwa kwa ufasaha na matamshi bora.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia suala la matamshi bora.

| 8.0 NDEGE NIMPENDAYE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Ufasaha** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa **(/mbw/,/nd/**, /**ny**/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 53 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi),<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo kwa ufasaha. | Je, ni kwa nini tunasoma kwa ufasaha? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kwa ufasaha.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali kusoma hadithi kwa ufasaha.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.
- Ubunifu – mwanafunzi anapojadiliana na wenzake na kusoma kifungu chepesi kwa ufasaha.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa kikundi.<br>● Upendo – mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia. |
| **Masuala Mtambuko**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika,kasi ifaayo na ishara zifaazo.<br>• Elimu ya utunzaji wa wanyama – mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Indigenous Language Activities na English Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufasaha. |

| **8.0 NDEGE NIMPENDAYE** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Tahajia**<br>(*Vipindi3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tahajia sahihi za maneno katika insha,<br>b) kuandika insha akizingatia tahajia sahihi za maneno,<br>c) kufurahia kutumia tahajia sahihi katika maandishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua tahajia sahihi za maneno katika uandishi wa insha kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kujadili kuhusu tahajia sahihi ya maneno katika kifungu kitabuni au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika insha akizingatia tahajia sahihi za maneno katika uandishi,<br>● kurekebisha insha akizingatia tahajia za maneno,<br>● kumsomea mzazi au mlezi | Kwa nini ni muhimu kuendeleza maneno ipasavyo unapoandika chochote? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | insha aliyoiandika kwa kuzingatia tahajia za maneno. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunza tahajia sahihi za maneno katika insha.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji wa tahajia sahihi za maneno katika insha.
- Ubunifu – mwanafunzi anapofaulu kuandika insha kwa kuzingatia tahajia za maneno.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Uwajibikaji – mwanafunzi anapoandika insha akizingatia tahajia sahihi.

**Masuala Mtambuko**

Elimu ya utunzaji wa wanyama – mwanafunzi anapojifunza kuandika insha kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za uandishi na tahajia sahihi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia matumizi ya tahajia za maneno.

DRAFT

## 8.0 NDEGE NIMPENDAYE

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4.Sarufi** | **8.4.1 Matumizi ya neno hili** na **haya** (*Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya neno **hili** na **haya** katika kifungu,<br>b) kutumia neno **hili** na **haya** katika kifungu ili kuboresha mawasiliano,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **hili** na **haya** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya neno **hili** na **haya** *(k.v. jicho hili – macho haya, jino hili – meno haya n.k.)* katika kifungu kwenye chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusoma sentensi zinazoonyesha matumizi ya neno **hili** na **haya** katika kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia neno **hili** na **haya** akiwa na wenzake,<br>● kuandika kifungu kwa kutumia neno **hili** na **haya** na kujadili na wenzake ili kukitolea maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu alichokitunga ili akitolee maoni. | Ni maneno yapi yanayoambatanishwa na maneno **hili** na **haya**? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapojenga msingi wa kujifunza zaidi kuhusu neno **hili** na **haya**.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia matumizi ya neno **hili** na **haya**.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapotumia neno **hili** na **haya** kurejelea vitu katika mazingira yake.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia neno **hili** na **haya** ipasavyo
- Amani – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali na wenzake ili kutambua na kutunga sentensi akitumia **hili** na **haya** kwa utulivu.

DRAFT

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya utunzaji wa wanyama – mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maneno lengwa.<br>● Mshikamano wa kijamii na kitaifa – mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kutambua matumizi ya **hili** na **haya**. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language activities – masomo haya pia yanashughulikia kuhusu vionyeshi. |

DRAFT

| 9.0 SOKONI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua suala lengwa linalozungumziwa,<br>b) kuzingatia matamshi bora katika mazungumzo,<br>c) kujieleza kwa ufasaha kuhusu suala lengwa,<br>d) kutumia ishara zifaazo katika mazungumzo,<br>e) kuchangamkia mazungumzo katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua suala lengwa linalozungumziwa kupitia kwa picha kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali pamoja na wenzake,<br>● kuchukua muda wa kufikiri kuhusu suala la kuzungumzia,<br>● kupanga mawazo yake kuhusu suala lengwa na kuandaa hoja za kuzungumzia,<br>● kutamka maneno kwa kuzingatia matamshi yafaayo ya sauti mbalimbali,<br>● kueleza habari ambayo zinaleta maana na zenye kufuatana vizuri,<br>● kupandisha na kushusha sauti panapohitajika,<br>● kutumia ishara mbalimbali zinazohusina na maelezo yake kuhusu suala lengwa,<br>● kuzungumza na mzazi au mlezi wake akizingatia suala lengwa ili aimarishe mawasiliano | Je,unazingatia nini unapozungumza kuhusu masuala mbalimbali? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki  mazungumzo na wenzake katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali kusikiliza mazungumzo.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo ya kila siku ili kuimarisha mawasiliano.
- Kujiamini – mwanafunzi anapojieleza kwa ufasaha mbele ya wenzake.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwenye kikundi.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali na nyenzo nyinginezo anazotumia kujifunzia.<br>● Heshima – mwanafunzi anapowasikiliza wenzake darasani na kuheshimu maoni yao. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Elimu ya kifedha – mwanafunzi anaposikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulika kusoma.<br>● Mathematics Activities – somo hili pia linashughulikia utumiaji wa pesa. |

DRAFT

| 9.0 SOKONI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.2. Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia picha,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya hadithi ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi kutoka kwenye chati, kadi maneno, mti maneno au kifaa cha kidijitali,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 70- 75 na kutambua msamiati wa suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa na kujadili ujumbe. | Je, ni mambo yapi unayozingatia unaposoma kifungu chochote? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapofanya utabiri kutokana na picha.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali kusoma hadithi.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili ujumbe na kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi katika kikundi.<br>● Heshima – mwanafunzi anapowaheshimu wenzake kushirikiana katika kusoma kifungu darasani.<br>● Upendo – mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya kifaa cha kidijitali darasani. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Elimu ya fedha – mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activies na Indigenous Language activities – masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa insha. |

DRAFT

/

| 9.0 SOKONI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Insha ya Masimulizi**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kati ya maneno 85-90 akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kuchangamkia uandishi wa insha ya masimulizi ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza masimulizi yakitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali,<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya masimulizi kutoka kwenye masimulizi aliyosikiliza,<br>● kusoma kielelezo cha insha ya masimulizi kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali kuhusu insha ya masimulizi akiwa na wenzake,<br>● kutambua mambo muhimu katika uandishi wa insha *k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko* katika kielelezo cha insha aliyosoma,<br>● kuandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa; kisa hiki kifuate hatua za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kisa kifupi kuhusu suala lengwa ili akitolee maoni. | 1. Je, unapenda kusimulia kuhusu nini?<br>2. Je,kisa ulichowahi kusimuliwa kilikuwa na mafunzo gani? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili vipengele vya uandishi wa insha.<br>● Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapoandika kifungu cha masimulizi akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Uwazaji wa kina – mwanafunzi anapotambua mambo yanayotakikana katika uandishi wa insha ya masimulizi.<br>● Ubunifu – mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia vipengele husika. | | | | |
| **Maadili**<br>● Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kikundi.<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia. | | | | |

DRAFT

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi – mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya masimulizi inayolenga mazingira ya sokoni.<br>● Elimu ya kifedha – mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.<br>● Matumizi ya dawa za kulevya – mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu matumizi ya dawa za kulevya zinazopatikana sokoni. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>English Language Activies na Indigenous Language activities – masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa insha. |

DRAFT

| 9.0 SOKONI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Matumizi ya juu ya, ndani ya, na mbele ya** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika kifungu,<br>b) kutumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika matini,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** kutoka kwa mgeni mwalikwa, mwalimu au vifaa vya kidijitali na kutambua matumizi yazo akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu kilichotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kujadili na mwenzake matumizi ya **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya** katika kifungu ili kutolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zilizotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kuigiza matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake kwa kutumia vitu anavyomiliki k.m; *Mboga iko ndani ya gunia,Vitabu viko juu ya rafu, Kitabu kiko ndani ya mkoba, Gari liko mbele ya duka,*<br>● kumtungia mzazi au mlezi wake sentensi kwa kutumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** kwa kuzingatia vitu katika mazingira ya nyumbani. | Je, ni maneno yapi unayoweza kutumia kurejelea kitu/mtu aliye mahali fulani? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapotoa mchango wake katika shughuli za kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia **juu ya**, **ndani y**a na **mbele ya.**

| |
|---|
| <ul><li>Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza kifungu au wimbo na vilevile anapofanya zoezi kwa kutumia tarakilishi.</li><li>Kujiamini – mwanafunzi anapowatungia wenzake sentensi kwa kutumia **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya.**</li></ul> |
| **Maadili**<ul><li>Heshima – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi huku akiyathamini maoni na michango ya wenzake.</li><li>Uwajibikaji – mwanafunzi anapotoa mchango wake katika kikundi na pia anapotangamana na vifaa vya kidijitali.</li><li>Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.</li><li>Amani – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi kwa utulivu.</li></ul> |
| **Masuala Mtambuko**<br>Elimu ya kifedha – mwanafunzi anapoigiza uuzaji na ununuzi akitumia juu ya,ndani ya na mbele ya. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigeneous Language Activitites – masomo haya pia yanashughulikia vihusishi. |

**10.0 TEKNOLOJIA**

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno na kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye silabi za sauti lengwa ili kufanikisha mawasiliano,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (/**mb**/, /**nz**/, /**tw**/) katika kitabu, kadi maneno, chati, mti maneno au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa (*km mboga, mbuzi, mbao, nzuri, mwanafunzi, twende, kutwa, katwa*) akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kwa sauti kifungu kifupi kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kujirekodi akisoma kifungu | Je, ni kwa nini tunatumia matamshi bora tunapozungumza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kilicho na maneno yaliyo na sauti lengwa akisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kifupi kwa kuzingatia silabi za sauti lengwa kwa matamshi bora. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini – mwanafunzi anapotamka maneno yenye silabi za sauti lengwa ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu chenye maneno ya sauti lengwa ili waitathmini na wenzake.

**Maadili**

- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake wakisikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa.

**Masuala Mtambuko**

Usalama mtandaoni – mwanafunzi anapotambua silabi za sauti lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia suala la matamshi bora.

## 10.0 TEKNOLOJIA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Ufasaha** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>d) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa (/mb/, /nz/,/tw/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 55 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi),<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake ,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | Kwa nini ni muhimu kusoma kifungu kwa ufasaha? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali.
- Kujiamini – mwanafunzi anaposoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,kasi ifaayo,sauti inayosikika na ishara zinazofaa.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Heshima – mwanafunzi anapothamini usomaji wa wenzake darasani.<br>● Upendo – mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani .<br>● Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Usalama mtandaoni – mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali inayohusu suala lengwa,awajibike na kuzingatia hatua za kiusalama.<br>● Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anaposoma hadithi kuhusu suala lengwa pamoja na wenzake kutoka jamii mbalimbali. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Indigenous Language Activities na English Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufahamu. |

| **10.0 TEKNOLOJIA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Insha ya Maelezo**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vinavyozingatiwa katika uandishi wa insha ya maelezo,<br>b) kuandika insha ya maelezo kati ya maneno 85-90 akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kuchangamkia kuandika insha ya maelezo ipasavyo ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya maelezo *(k.v wahusika, ujumbe, muundo )* kwenye kitabu, kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maelezo yakitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kielelezo cha insha ya maelezo kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutambua kanuni za uandishi wa insha ya maelezo (*k.v. mwandiko nadhifu, mtiririko)* akiwa na wenzake,<br>● kuandika insha ya maelezo kuhusu suala | Je,unatumia maneno ya aina gani unapotoa maelezo kuhusu kitu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | lengwa kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa insha ya maelezo na kuwasomea wenzake ili waitolee maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi insha ya maelezo aliyoandika. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya maelezo.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anaposikiliza insha ya maelezo kutoka kwa kifaa cha kidijitali.
- Ubunifu – mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia vipengele vifaavyo.

**Maadili**

- Upendo – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Heshima – mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

Usalama mtandaoni – mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa akizingatia hatua za uandishi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

English Language Activities na Indigenous Languages – masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa insha ya maelezo.

DRAFT

**10.0 TEKNOLOJIA**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Vitendo** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vitendo katika matini,<br>b) kutumia vinyume vya vitendo ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vitendo na vinyume vyake katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vinyume vya vitendo (*k.v. fungua-funga, keti- simama, twika- tua)* kwenye chati, kitabu au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu chenye vinyume vya vitendo kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusoma vinyume vya vitendo katika kifungu akiwa na wenzake,<br>● kukamilisha sentensi akitumia vinyume vya vitendo akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake,<br>● kumtajia mzazi au mlezi vinyume vya maneno alivyojifunza darasani. | Je, unajua vinyume vipi vya vitendo? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika vinyume vya vitendo katika sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya vinyume vya vitendo.
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo.

**Maadili**

- Uwajibikaji – mwanafunzi anapotekeleza shughuli ipasavyo.
- Umoja – mwanafunzi anapofanya kazi pamoja na wenzake kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Mshikamano wa kijamii – mwanafunzi anapoigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake kutoka jamii tofauti tofauti bila ubaguzi.

DRAFT

| |
|---|
| ● Usalama mtandaoni – mwanafunzi anapotambua vinyume vya vitendo katika kifungu kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kuzingatia hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>English Language Activities na Indigenous Language Activities – masomo haya pia yanashughulikia vinyume. |

DRAFT

**KIAMBATISHO 1: MWONGOZO WA KUTATHMINIA STADI ZA LUGHA GREDI YA 3**

| **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**<br>**Vigezo na viwango vya kutathmini** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango**<br><br>**Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali Na Matarajio** |
| **Kuweza kuwasiliana kwa njia ifaayo** (*matamshi, kiimbo na kusikika*) | Mwanafunzi anajieleza kwa ufasaha na utendeti, bila makosa ya kimatamshi ya sauti lengwa na anapozungumza anasikika ipasavyo na asemayo yanaeleweka vyema. Maelezo yake yana mantiki na yanafuatilika kwa urahisi. Anazungumza kama mzawa wa lugha hii. | Mwanafunzi anajieleza kwa ufasaha. Ana matamshi yafaayo yanayozingatia sauti lengwa . Aidha ana kiimbo mwafaka. Ana makosa machache ya kimatamshi na kiimbo lakini anasikika vyema na asemayo yanaeleweka. | Mwanafunzi anajieleza kwa kusitasita. Anafanya makosa ya kimatamshi yanayotokana na sauti lengwa na kiimbo chake kina udhaifu. Mara kwa mara na hasisikiki vyema. Maana inaweza kukisiwa kutokana na asemayo. | Ana stadi hafifu za kimatamshi na kiimbo. Anafanya makosa mengi ya kimatamshi. Anakosa mantiki /mfuatano ufaao katika kujieleza. Hasisikiki vyema na asemayo hayaeleweki. |
| **Kufahamu suala lengwa** (*majibu sahihi, matumizi ya msamiati mwafaka*) | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa kwa mfano katika ufahamu wa kusikiliza. Anatoa majibu sahihi kwa maswali yote aliyoulizwa kwenye muktadha. Anautumia msamiati mpana wa mada lengwa kwa usahihi. | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa kwa mfano katika ufahamu wa kusikiliza. Anatoa majibu sahihi kwa idadi kubwa ya maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. Anatumia msamiati lengwa ipasavyo k.m hiki na hivi. | Anatoa maelezo kwa baadhi ya maswali katika muktadha wa suala lengwa kwa mfano katika ufahamu wa kusikiliza. Anatoa majibu kwa baadhi ya maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. Anatumia baadhi ya msamiati wa suala lengwa. | Ana changamoto kujibu maswali aliyoulizwa kutokana na ufahamu wa kusikiliza. Anautumia msamiati finyu wa mada lengwa. |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kutumia msamiati wa suala lengwa** *(msamiati wa heshima, adabu, maamkuzi, maagano, n.k)* | Anatumia msamiati mbalimbali kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. Kwa mfano hiki na hivi. | Anatumia msamiati mwafaka kulingana na muktadha/suala lengwa. Kwa mfano hiki na hivi. | Anatumia msamiati mchache kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. Kwa mfano hiki na hivi. | Anatumia msamiati wa mada lengwa kwa kutatizika ana changamoto kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. |
| **Kutumia ishara za mwili ipasavyo (***jinsi anavyoketi/kusimama, ishara uso, kumtazama mwalimu,ukakamavu)* | Anaketi/ kusimama na kutumia ishara za uso na mwili ipasavyo. Anamtazama mwalimu kila wakati kwa nia ya kuwasilisha ujumbe na anazungumza kwa ukakamavu. | Anaketi/ kusimama na kutumia ishara za uso na mwili ipasavyo. Anamtazama mwalimu wakati mwingi kwa nia ya kuwasilisha ujumbe na anazungumza kwa ukakamavu. | Anaketi/kusimama na kutumia baadhi ya ishara za uso na mwili. Anamtazama mwalimu mara kwa mara na anazungumza kwa kusitasita. Baadhi ya nyakati anazungumza kwa ukakamavu. | Ni nadra sana kutumia ishara za uso na mwili. Hamtazami mwalimu kabisa. Anaangalia chini au kando akizungumza. |

**KUSOMA**
**Vigezo na viwango vya kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali Na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kuzingatia jinsi ya kuketi na mbinu zifaazo wakati wa kusoma. *(kuketi wima, kushika kitabu ipasavyo, kuelekeza macho kutoka kushoto hadi kulia n.k)* | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kusoma. Anatumia vifaa vya kusomea kwa namna ifaayo bila ugumu wowote. Anatumia ishara za mwili kwa njia mwafaka anaposoma kwa wepesi. | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kusoma. Anatumia vifaa vya kusomea kwa namna ifaayo. Anatumia ishara za mwili kwa njia mwafaka anaposoma. | Anaketi jinsi ipasavyo wakati wa kusoma. Anatumia baadhi ya vifaa vya kusomea kwa namna ifaayo. Anatumia baadhi ya ishara za mwili kwa njia mwafaka anaposoma | Anachangamoto ya kuketi jinsi inavyofaa wakati wa kusoma. Anatumia baadhi ya vifaa vya kusomea kwa namna ifaayo kwa usaidizi. Anatumia ishara chache za mwili kwa njia mwafaka anaposoma |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kufahamu suala lengwa** (*majibu sahihi, matumizi ya msamiati mwafaka, anwani, picha na michoro*) | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa alilosoma kwenye matini kwa urahisi. Anatoa majibu sahihi kwa maswali yote aliyoulizwa kwenye muktadha. | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa alilosoma kwenye matini. Anatoa majibu sahihi kwa idadi kubwa ya maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha | Anatoa maelezo kwa baadhi ya maswali katika muktadha. Anatoa majibu kwa baadhi ya maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. | Anachangamoto kuelewa na kutoa maelezo kwa maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. |
| Kusoma kwa kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia kipengele cha ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha na urahisi. | Anasoma kwa kuzingatia kipengele cha ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele k.m ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu. | Anajaribu kusoma sehemu za kifungu bila kuzingatia kipengele cha ujumbe, matukio na wahusika. |
| **Kasi ya usomaji** (*Idadi ya maneno yanayosomwa kwa usahihi kwa muda wa dakika moja*) | Anasoma kwa urahisi na mfululizo wakati wote. Anatumia vituo/ alama za uakifishaji mahali panapofaa wakati wote anaposoma kifungu kuanzia mwanzo hadi mwisho. Anasoma kwa usahihi zaidi ya maneno **(55-60)** kwa muda wa dakika moja. | Anasoma kwa urahisi na mfululizo. Anatumia vituo/ alama za uakifishaji mahali panapofaa katika kiasi kikubwa cha muda wa kusoma. Anasoma kwa usahihi idadi ifaayo ya maneno **(55-60)** kwa muda wa dakika moja. | Wakati mwingine anasitasita anaposoma. Hazingatii kikamilifu vipumuo na vikomo mwishoni mwa sentensi. Anasoma kwa usahihi kati ya maneno **(28-30)** kwa muda wa dakika moja. | Anatatizika kusoma na anarudiarudia maneno mengi na inabidi kurudi nyuma kuanza upya. Anachosoma hakiwezi kufuatilika. Anasoma kwa usahihi kati ya maneno **(14-15)** kwa muda wa dakika moja. |

**KUANDIKA**
**Viwango na vigezo vya kutathmini**

| Viwango | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|

| Vigezo | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika sentensi , kifungu kifupi au insha kwa kuzingatia mada lengwa na maagizo mengine yaliyotolewa. | Anaonyesha ubunifu na uasilia mkubwa katika uandishi wa sentensi kwa kuzingatia mada lengwa.<br>Anafikisha idadi ya maneno aliyopewa (85-90) na kuzidisha. | Anaandika sentensi kwa ubunifu kwa kuzingatia mada lengwa. Anafikisha idadi ya maneno aliyopewa (85-90) | Anaandika sentensi kwa ubunifu kwa kuzingatia mada lengwa.<br>Anafikisha idadi ya maneno aliyopewa (43-45) | Ana changamoto kuandika sentensi kwa kuzingatia mada lengwa.<br>Anafikisha idadi ya maneno aliyopewa (22-23) |
| Kuzingatia sarufi na ufundi wa uandishi | Anadhihirisha umilisi wa kiwango cha juu cha sarufi, uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wake. | Anatumia sarufi, alama za uakifishaji na kuendeleza maneno ipasavyo katika uandishi. Hata hivyo, ana makosa machache ambayo hayatatizi usomaji. | Ana makosa ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno ambayo yanatatiza usomaji wa sehemu za insha yake. | Ana makosa mengi ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno kuanzia mwanzo hadi mwisho wa uandishi.<br>Msomaji anaweza tu kukisia maana. |
| Kuandika kwa hati nzuri | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.<br>Anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari.<br>Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno kutoka mwanzo hadi mwisho wa insha. | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.<br>Anatenganisha herufi nyingi ipasavyo.<br>Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno. | Ana mwandiko usio nadhifu lakini unasomeka.<br>Anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo.<br>Anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno. | Ana mwandiko usiosomeka kwa urahisi.<br>Hatenganishi herufi nyingi ipasavyo.<br>Anaacha nafasi nyingi zisizolingana baina ya maneno. |
| Msamiati | Ana uteuzi mzuri wa maneno na matumizi anuwai ya msamiati | Ana uteuzi mzuri wa msamiati anaoutumia | Anatumia msamiati finyu ambao wakati mwingi haulingani na | Anatumia msamiati finyu ambao haulingani na muktadha |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kulingana na muktadha wa sentensi. | katika kutunga sentensi. | muktadha wa sentensi. | wa sentensi. |
| Kuzingatia muundo na mtindo wa kuandika aya ( *nafasi ya pambazo,idadi ya maneno)* | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika aya isiyozidi maneno 60 | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika aya isiyozidi maneno aliyopewa (yasiyozidi 60) | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika aya. Anazidisha maneno aliyopewa (60) | Anachangamoto kuzingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika aya. Hafikishi maneno 60. |

**SARUFI**
**Vigezo na viwango vya kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidi Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali Na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kutambua aina za maneno katika lugha ya Kiswahili *(yeye, wao, yule, wale, hili na haya n.k)*** | Anatambua aina za maneno aliyofunzwa katika matini alizopewa kwa wepesi | Anatambua aina za maneno aliyofunzwa katika matini alizopewa | Anatambua aina za maneno aliyofunzwa katika matini alizopewa. | Anachangamoto kutambua aina za maneno aliyopewa katika matini alizopewa. |
| **Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno aliyofunzwa** | Anatunga sentensi sahihi kwa kuzingatia maneno aliyofunzwa kwa wepesi | Anatunga sentensi sahihi kwa kuzingatia maneno aliyopewa kwa ipasavyo. | Anatunga baadhi ya sentensi sahihi kwa kuzingatia maneno aliyopewa. | Anatunga baadhi ya sentensi sahihi kwa kuzingatia maneno aliyopewa kwa kuelekezwa |
| **Kutumia lugha kwa usahihi** *(uakifishaji, ukanushaji wa nafsi ya pili, umoja, wingi, udogo wa sentensi, vinyume vya vitendo n.k)* | Anazingatia kanuni za lugha ipasavyo katika matini kwa utendeti. | Anazingatia kanuni za lugha ipasavyo katika matini. | Anazingatia baadhi ya kanuni za lugha ipasavyo katika matini. | Anazingatia kanuni baadhi y kanuni za lugha ipasavyo katika matini kwa kuelekezwa. |

**KIAMBATISHO 2: SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL)**

Katika kiwango hiki, lengo la shughuli ya CSL ni kuambatanisha dhana zilizofunzwa darasani katika masomo mbalimbali na tajriba za maisha halisi. Huwawezesha wanafunzi kuona jinsi mambo waliyojifunza yanavyohusiana na maisha ya kila siku. CSL huwa katika somo la *Environmental Activities*. Mwalimu darasani anatarajiwa kutambua na kuwaelekeza wanafunzi kutekeleza shughuli ya CSL ya darasa zima na jumuishi inayofaa kulingana na umri wa wanafunzi ndani ya shule. Usalama wa wanafunzi unafaa utiliwe maanani wakati wa kuchagua shughuli hii. Zifuatazo ni hatua za shughuli ya CSL jumuishi ambayo inafaa itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula wa shule.

| |
|---|
| **1. Hatua za Utekelezaji wa Shughuli ya Huduma ya Kijamii Inayochangia Ujifunzaji (CSL)** |
| **2. Maandalizi**<br>• Amua shughuli itakayotekelezwa na wanafunzi.<br>• Tambua umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo mahususi kwa shughuli ya CSL.<br>• Tambua nyenzo hitajika kwa shughuli hiyo (vifaa vinavyopatikana karibu).<br>• Panga shughuli hiyo itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula (weka tarehe na saa ya shughuli).<br>• Wasiliana na wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule, walimu na wadau wengine katika jamii ya shule.<br>• Tambua na ukuze vifaa vya kutathminia. |
| **3. Utekelezaji wa Shughuli ya Huduma ya Kijamii Inayochangia Ujifunzaji (CSL)**<br>• Wapatie wanafunzi majukumu.<br>• Hakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki katika shughuli hii.<br>• Watazame wanafunzi wanapotekeleza shughuli ya CSL na uweke rekodi ya matokeo.<br>• Tumia kifaa kifaacho cha tathmini kutathmini mchakato wa shughuli na matokeo (tathmini kazi ya wanafunzi kutoka mwanzo hadi mwisho).<br>• Tathmini umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo. |
| **4. Utafakuri wa Utekelezaji wa Shughuli ya Huduma ya Kijamii Inayochangia Ujifunzaji (CSL)**<br>Kuwa na muda wa tathmini binafsi na wanafunzi kuhusu shughuli waliyotekeleza ya CSL jumuishi kwa kujadili yafuatayo:<br>• Ni nini kilifanyika vyema na kwa nini.<br>• Ni nini ambacho hakikufanyika vizuri na kwa nini.<br>• Ni nini kinachoweza kufanywa kwa njia tofauti wakati ujao.<br>• Ni nini wanafunzi walijifunza. |

Kutakuwa na shughuli moja ya CSL kwa mwaka. Masuala makuu ya CSL jumuishi yatatokana na kategoria pana za masuala mtambuko na ujuzi unaolengwa katika masomo mbalimbali. Walimu wanatarajiwa kuwa na masuala tofautitofauti yanayolengwa kila mwaka ili kuwapa fursa

wanafunzi kutalii masuala mtambuko mbalimbali. Kunafaa kuwa na uhusiano kati ya stadi za masomo na masuala makuu.

Shughuli ya CSL itakuwa ya shule nzima ambapo jamii yote ya shule itahusika (wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule na walimu). Wazazi/walezi ni washikadau muhimu katika kupanga na kutekeleza shughuli ya CSL. Ingawa walimu huongoza upangaji na utekelezaji wa shughuli ya CSL, wanafunzi watatarajiwa kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima.

Shughuli hii ya CSL hutoa fursa ya ukuzaji wa umilisi wa kimsingi na maadili mbalimbali. Mwalimu anatarajiwa kulenga umilisi na maadili tofautitofauti.

## 5. Tathmini ya Shughuli ya Huduma ya Kijamii Inayochangia Ujifunzaji (CSL)

Tathmini ya CSL jumuishi italenga vipengele 3 ambavyo ni: stadi kutokana na masomo mbalimbali yatakayojumuishwa katika shughuli hii, umilisi wa kimsingi uliokuzwa na maadili yaliyokuzwa. Tathmini inafaa kulenga mchakato mzima wa utekelezaji na matokeo ya mwisho ya shughuli. Mwalimu atatathmini wanafunzi katika vikundi akitumia vifaa mbalimbali kama vile ratiba ya ukaguzi, orodha hakiki, kiwango cha ukadiriaji na vifaa vingine faafu vya tathmini.

## KIAMBATISHO 3: MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI

| Mada | Mbinu za Kutathminia Zilizopendekezwa | Nyenzo za Kufundishia Zilizopendekezwa | Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji Zilizopendekezwa |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>e) Kuambatanisha maneno na majibu<br>f) Mijadala<br>g) Mazungumzo<br>h) Matumizi ya ishara za mwili k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>i) Wanafunzi wanatathminiana. | · Chati<br>· Michoro na picha<br>· Mgeni mwalikwa<br>· Vifaa vya kidijitali (k.v tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>· Mti maneno<br>· Kapu maneno<br>· Vitabu mbalimbali | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| KUSOMA | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati wa suala lengwa<br>b) Kujibu maswali k.m. katika ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kukariri na kuimba mashairi<br>e) Kusoma kwa sauti<br>f) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>g) Potfolio<br>h) Shajara | · Tarakilishi/vipakatalishi<br>· Kinasasauti<br>· Rununu<br>· projekta<br>· Tarakilishi/vipakatalishi<br>· Kinasasauti<br>· Rununu<br>· projekta<br>· Nakala ya shairi<br>· Kamusi mbalimbali | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |

| Mada | Mbinu za Kutathminia Zilizopendekezwa | Nyenzo za Kufundishia Zilizopendekezwa | Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji Zilizopendekezwa |
|---|---|---|---|
| KUANDIKA | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potfolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | · Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>· Kielelezo cha insha ya maelezo<br>· Kielelezo cha insha ya wasifu<br>· Nakala ya barua ya kirafiki<br>· Nakala ya barua rasmi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| SARUFI | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno lengwa<br>c) Kujaza nafasi<br>d) Kujaza fumbo maneno<br>e) Kazi mradi | · Tarakilishi/vipakatalishi<br>· Kinasasauti<br>· Rununu<br>· projekta<br>· Kapu maneno<br>· Mti maneno<br>· Kadi za maneno<br>· Picha za vitu mbalimbali<br>· Michoro<br>· Chati<br>· Mabango<br>· Sanamu<br>· Nyenzo halisi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Ziara za nyanjani<br>4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |

DRAFT

DRAFT

DRAFT